

TUME YA PAMOJA YA FEDHA

MAELEZO MAFUPI YA MAJUKUMU YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TUME YA PAMOJA YA FEDHA KWA MWAKA 2020/21 NA 2021/22

katika mwaka 2020/21, Tume ya Pamoja ya Fedha ilieendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Ibara 133 na 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kutoa ushauri ya Uhusiano wa Kifedha baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Katika kutekeleza majukumu hayo, Tume ilifanya stadi kuhusu Mwenendo wa Ukuaji wa Sekta za Kiuchumi na Mapato ya Muungano kwa lengo la kubainisha changamoto zinazoweza kuathiri mapato ya Muungano. Uchambuzi wa Stadi hiyo umebaini kuwa kiwango cha biashara baina ya pande mbili za Muungano kimeongezeka kwa wastani wa tani 283.6 au asilimia 85.4 katika kipindi cha mwaka 2009 hadi 2018. Aidha, changamoto kadhaa zilibainika katika maeneo ya ushirikiano wa kibiashara. Vilevile, Tume ilifanya uchambuzi wa takwimu za Mapato na Matumizi ya Muungano kwa mwaka 2018/19, 2019/20 na 2020/21.

Katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Tume katika kutekeleza jukumu lake kuu la kushauri na kutoa mapendekezo kuhusu kuimarisha uhusiano wa kifedha baina ya SMT na SMZ, Tume ya Pamoja ya Fedha imepanga kufanya

- i. Stadi Kuhusu Ukusanyaji wa Mapato ya Muungano yanayotokana na Biashara ya Huduma kati ya Tanzania Bara na Zanzibar. Stadi

hiyo inalenga kubainisha changamoto na fursa zilizopo, na athari zake katika mapato ya Muungano.

- ii. Kuendelea kufanya uchambuzi wa Mapato na Matumizi yanayohusu utekelezaji wa Mambo ya Muungano kwa Mwaka 2019/20, 2020/21 na 2021/22, na ;
- iii. Kutoa elimu kwa wadau kuhusu Uhusiano wa Kifedha baina ya pande mbili za Muungano.